

MAKAO MAKUU

**Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania**

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa
Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania)**

TAARIFA inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni ya uzalishaji umeme kutoka kwa Kampuni ya Kilombero Plantations Limited. EWURA inakaribisha maoni na pingamizi kuhusiana na maombi haya. Taarifa za muombaji pamoja na aina ya leseni iliyoombwa ni kama ifuatavyo:

Na.	MAELEZO
Jina na anuani ya Mwombaji	M/s. Kilombero Plantations Limited , P. O. Box 23294, Dar es Salaam.
Eneo	Kata ya Mngeta, Wilaya ya Kilombero, Mkoa wa Morogoro.
Taarifa za Wanahisa	1) Agrica Tanzania Limited (formerly InfEnergy Tanzania Limited), S. L. P 78934, Dar es Salaam, 50% . 2) Rufiji Basin Development Authority, S. L. P 9320, Dar es Salaam, 50% .
Maelezo ya Mtambo na Matumizi	Kituo kina uwezo wa kuzalisha umeme kwa kiwango cha Megawati 1.692, zinazohusisha jenereta moja yenye uwezo wa kuzalisha kW 500 kwa kutumia tungamotaka, jenereta mbili zenye uwezo wa kuzalisha kW 400 kila moja kwa matumizi ya dharura, jenereta mbili zenye uwezo wa kuzalisha kW 160 kila moja kwa kutumia maji na jenereta moja ya kW 72 kuzalisha umeme kwa kutumia diseli kwa ajili ya kuendesha mitambo inayozalisha umeme kwa kutumia tungamotako. Umeme utakaozalishwa utatumika kwenye mashamba ya mpunga yanayomilikiwa na kampuni ya Kilombero Plantations Ltd.
Aina na Muda wa Leseni	Leseni ya kuzalisha umeme kwa kipindi cha Miaka Kumi na Tano

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusiana na maombi haya awasilishe kwa maandishi kabla ya saa 10 jioni, siku ya tarehe 16 Mwezi Agosti 2018. Maombi ya leseni yanaweza kuonyeshwa kwa mtu kwa maombi maalum ya maandishi.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu